

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MKOA: LINDI

SIMU: 0762525986

0789809128

0717927797

0682455396

KUMB. NA.C.6/KSS/VOL.III/98



SHULE YA SEKONDARI YA KILWA

S.L.P. 171,

KILWA MASOKO.

14 - 12 - 2020

MZAZI/MLEZI WA.....

C/O MWALIMU MKUU

SHULE YA MSINGI.....

S. L. P 4

KILWA - MASOKO

YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO

KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI KILWA KWA MWAKA 2021.

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika **Shule ya Sekondari Kilwa** kwa mwaka wa masomo **2021**.

Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni fursa kubwa na ya pekee kwake aliyo pewa na serikali ya Tanzania.

Shule ya Sekondari Kilwa ni shule ya kutwa, ipo **Mkoa wa Lindi** katika **wilaya ya Kilwa**.

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**, hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021**.

Napenda kukusisitiza kufanya maandalizi mapema juu ya mahitaji ya mwanao ili aweze kuripoti kwa wakati na kuwahi masomo sambamba na wenzake kwani kutofanya hivyo itakuwa ni kumkosesha haki yake ya kupata elimu. Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ili uzishughulikie haraka na kuzirejesha shuleni mapema iwezekanavyo au siku ya kuripoti.

- Mambo muhimu ya kuzingatia
- Fomu ya kupima afya ya mwanafunzi
- Taarifa ya mwanafunzi na mzazi /mlezi

KARIBU SANA KILWA SEKONDARI

JASON G KASHIAJA.

MKUU WA SHULE

FOMU NA 2: MAMBO MUHIMU YAKUZINGATIA

A. MAHITAJI YA LAZIMA YA SHULE

- 1.Picha za rangi NNE (passport size) zipigwe akiwa amevaa sare za shule. (shati jeupe).
- 2.Madaftari ya kutosha yapatayo 10 kwa masomo tisa ya msingi na 1 ziada.
- 3.Nakala ya cheti cha kuzaliwa

B: SARE YA SHULE

(a)Wavulana sare zao ni

- (i) Suruali mbili za khaki zenye malinda mawili (zenye upana wa kutosha zisizobana makalio wala miguu)
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi, buti haziruhusiwa.
- (iv) Soksi ndefu (stockings) nyeupe jozi mbili

(b)Wasichana Sare zao ni

- (i) Sketi mbili za kijani ndefu mpaka juu ya kifundo cha mguu)
- (ii) Mashati mawili meupe mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu tu
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu.
- (iv) Soksi ndefu (stockings) nyeupe jozi mbili
- (v) Wanafunzi wasichana wanaruhusiwa kuvaa **HIJABU** ndefu nyeupe yenye mishono ya duara usoni na **nusu kanzu**.
- (vi) Viatu vyeusi visiwe vya rangi rangi, madoa doa; mistari ya mapambo na visigino virefu.

C: VIFAA VYA USAFI NA MAZINGIRA

Kila mwanafunzi atatakiwa kuja na vifaa vya usafi kama ifuatavyo:-

- 1. Jembe lenye mpini na fyekeo.
- 2. Ufagio mmoja (wa kusimama uliotengenezwa kwa makuti ya mnazi)
- 3. Sabuni ya maji lita moja kwa ajili ya usafi

4. Mche mmoja wa mti wa matunda(mchungwa/mwembe/parachichi/staferi/mpera nk)

D: TAARIFA ZA MWANAFUNZI

- 1.(a)Jina la mwanafunzi
- (b)Tarehe ya kuzaliwa Mwezi Mwaka
- (c).Shule aliyomalizia darasa la saba..... Mwaka
- 2.Jina kamili la Mzazi/Mlezi
- 3.Jina kamili la baba.....(HAI/AMEFARIKI)
- 4.Jina la mama..... (HAI/AMEFARIKI)
- 5.Kazi za wazazi : (i)Baba.....(ii)Mama.....
- 6.Idadi ya ndugu wa kiume.....Idadi ya ndugu wa kike.....
- 5.Anuani ya mzazi/mlezi..... Namba ya simu
- 6.Mkoa Wilaya Tarafa
- 7.Kata Kijiji Mtaa
- Jina la Mzazi/Mlezi Sahihi Tarehe**

1. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- (i) Wizi
- (ii) Kutohudhiria masomo kwa Zaidi ya siku 60 bila taarifa/ utoro
- (iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
- (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
- (v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi au kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
- (vi) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- (vii) Uvutaji wa sigara
- (viii) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
- (ix) Kusababisha ujauzito au kutoa mimba
- (x) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- (xi) Kumiliki simu ya mkononi shuleni
- (xii) Kudharau Bendera ya Taifa
- (xiii) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
- (xiv) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya nakuyatekeleza kikamilifu

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENT
KILWA DISTRICT COUNCIL**

REGION: LINDI

PHONE: 0762525986
0672850728
0782336592



KILWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 171,
KILWA MASOKO.
08/12/2019.

KUMB. NA.C.6/KSS/VOL.III/98

FORM 2:

To the medical officer

.....
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school education as a student on the following grounds:

1. Pupil full name Age.....
2. Blood.....
3. Stool
4. T.B. Test
5. Syphilis
6. Urine examination
7. Eye test.....
8. Chest test.....
9. Ears test.....
10. Spleen
11. Abdomen.....
12. Pregnancy test (for girls only)

ANY ADDITIONAL INFORMATION E.g. physical defects or impairment, infection, family diseases, etc.....
.....

I certify that, the above named pupil is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons

.....
NAME OF MEDICAL OFFICER..... SIGNATURE AND STAMP.....